

Tumsifu Yesu Kristo!

Wapendwa waamini Wakatoliki, hasa wale wanaoteseka wanaposhuhudia Mama yetu Kanisa takatifu linaishi kupidia mgogoro na taabu usio wa kawaida. Ndugu zangu Baba na mama wa familia katoliki! Wapendwa vijana wa Kikatoliki! Wapendwa watoto wa Kikatoliki wasio na hatia! Na Masista wapendwa, lulu za kiroho za Kanisa! wapendwa waseminari wa Kikatoliki! Wapendwa makuhanani wa Kikatoliki, amba ni "upendo wa Moyo Mtakatifu wa Yesu"! Mkanganyiko na fujo ndani ya Kanisa umefikia hatua kwamba tunapaswa kumwomba Bwana kwa maneno ya Esta: "Hatuna msaidizi ila wewe" (Esta 4:31/14:3). Kwa hiyo, hebu tukimibilie katika Moyo Safi wa Maria kupidia Sala ya kila siku ya kuomba Mapapa watakatifu. Hebu tupige kelele na mtunga-zaburi: "Ondoka, Ee Bwana, kwa nini unalala? Simama, Ee Bwana, utusaidie na utuletee wokovu!" (Zab. 43:23).

Januari 18, 2024, Sikukuu ya Kale ya kitu cha ukuu wa Mtakatifu Petro huko Roma

+ Athanasius Schneider, Askofu Msaidizi wa Jimbo kuu la Bikira Maria wa Astana

Sala kwa ajili ya Kuomba Mapapa Watakatifu

Bwana utuhurumie! Kristu utuhurumie! Bwana utuhurumie! Bwana Yesu Kristo, Wewe ni Mchungaji Mwema! Kwa mkono wako wenye nguvu unaongoza Kanisa lako la linalohiji kupidia dhoruba za kila wakati na enzi.

Pamba Kiti kitakatifu na mapapa watakatifu ambao hawaogopi wenye nguvu wa ulimwengu huu wala hawafanyi mapatano na roho ya dunia hii, bali wana bidii kuhifadhi, kuimarisha, na kutetea Imani Katoliki hata kwa kumwaga damu yao, wakishika, kulinda, na kukabidhi kwa vizazi vijavyo liturujia ya heshima ya Kanisa la Roma

Ee Bwana, urudi kwetu kupidia mapapa watakatifu ambao, wakijawa na bidii ya Mitume, wanatangaza kwa ulimwengu wote: "Wokovu haupatikani katika mwengine isipokuwa katika Yesu Kristo. Kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu ambalo kwalo wanapaswa kuokolewa" (Taz. Matendo 4:10-12).

Kupitia kizazi cha mapapa watakatifu, Kiti kitakatifu - ambacho ni nyumbani kwa wote wanaoendeaza Imani ya Kikatoliki na ya Kitume—daima kiangaze kama makao ya ukweli kwa ulimwengu wote. Tusikilize sisi, Ee BWANA, na kwa njia ya maombezi ya Moyo Safi wa Maria, Mama wa Kanisa, tupe Mapapa watakatifu, tupe Mapapa wengi watakatifu! Utuhurumie na utusikilize! Amina.